**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**Namba za Simu**
Mkuu wa Shule : **0682008720**
Makamu Mkuu wa Shule: **0769672564**
Malezi: **0755859657**

**Shule ya Sekondari Pugu**
S.L.P 9090
**DAR ES SALAAM**
Tarehe................

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..........................................................................................
S.L.P. ..........................
..........................................

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PUGU HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA, MKOA WA DAR ES SALAAM, MWAKA 2018**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **Tano** katika shule hii mwaka **2018,** tahasusi ya..............
Shule ya Sekondari Pugu ipo umbali wa kilometa 18.6 kutoka stendi kuu ya mabasi ya mikoani Ubungo. Ukifika kituo cha mabasi Ubungo, panda gari ya kwenda Gongo lamboto. Nauli ni shilingi mia tano (500/=)Teremka Gongo lamboto, panda gari inayokwenda Kigogo fresh au Chanika nauli ni shilingi mia nne (400/=), teremka kituo cha Pugu Sekondari.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **02/07/2018.** Hivyo, Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **16/07/2018.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe..............

**2.1 Mwanafunzi aje na sare za shule kama ifuatavyo:**

(a) Suruali rangi ya **darkbluu mbili,** mashati meupe ya mikono mifupi mawili, vesti nyeupe mbili zisizo na urembo wowote.
(b) Suruali ya shule inatakiwa iwe na marinda mawili, upana wa chini uwe ishirini na mbili (22). Iwe na turn up chini.
(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni Jezi Nyekundu(Bukta na T.shirt yake) **jozi mbili (02)** na viatu vya michezo.
(d) Viatu vya Shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi **jozi mbili**(02)
(e) Soski nyeusi jozi mbili (Zisizo na alama wala urembo wowote)
(f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.(mikanda miwili)
(g) Sweta mbili rangi ya dark bluu yenye shepu ya V shingoni.
(h) Nguo za kushindia(shamba dress); Mwanafunzi aje na suruali mbili za khaki zenye marinda mawili, upana wa chini uwe ishirini na mbili iwe na turn up.Shamba dress itavaliwa pamoja na T-shirt mbili ambazo zinapatikana shuleni kwa bei ya shilingi kumi na moja elfu na mia tano(11,500/=). Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni.

**2.2 Ada na Michango ya Shule**

**(a)(i)** Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= . unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba **20301100113** katika benki ya **NMB** (*tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip*).

**(ii) michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i) Kitambulisho na picha ni shilingi 6,000/=
ii) Taaluma ni shilingi 20,000/=
iii) Vibarua (Wapishi na Walinzi) ni shilingi 30,000/=
iv) Nembo ya shule ni shilingi 2,000/=
v) Matibabu ni shilingi 10,000/=(Mwenye Bima ya Afya atalipa shilingi 5,000/=)
vi) Mitihani ya kujipima(Mock) ni shilingi 20,000/=
vii) Kukodisha godoro kwa muhula ni shilingi 10,000/=
viii) Tahadhari ni shilingi 5,000/=

Fedha hizi zote zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba **20301100113** katika benki ya **NMB**

**(b) Mchango kwa ajili ya ukarabati wa samani shilingi 15,000/=** fedha hizi zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba **0150251320600** katika benki ya **CRDB**

**c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

(i) Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)
(ii) Vitabu vya masomo vya tahasusi husika.
(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa biolojia
(iv) Scientific calculator
(v) Godoro la sponji **moja** futi **mbili na nusu** lenye foronya.
(vi) Mashuka pair 2 rangi ya bluu bahari ( Light blue) futi 3/6, mto na foronya mbili ( rangi ya shuka) na chandarua 1
(vii) Vyombo vya Chakula (Bakuli, Sahani, Kijiko na Kikombe)
(viii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
(ix) Vifaa vya Usafi(Kwanja, Jembe, Reki, soft broom, Fagio ya chelewa,Mopper,dustbin)
(x) Taulo moja (1) mswaki, sabuni, na kanda mbili za kuogea pair 1
(xi) Sanduku la bati (1)
(xii) Picha nne(04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu. Mwanafunzi husika awe na passpot size (04) nne.

**3. Sheria na kanuni muhimu za shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

NB: Vifaa vya usafi vilivyotajwa kipengele (ix) viletwe kama ifuatavyo.
PCM – Jembe-1, Panga 1, chelewa 1
PCB – Soft broom-2, Squizzer 2
EGM – Mopper-1

### 3.1 HESHIMA

(i) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wote kwa mwalimu na watu wengine.

(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote shuleni walimu na wasio walimu kama walezi

(iv) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kuthamini kazi

(v) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:-
   (a) Kuvuta sigara/ulevi/ uasherati
   (b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na ndevu
   (c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
   (d) Kugombana na kupigana.

(vi) Mwanafunzi aitikie wito mara moja anapoitwa, mathalani kengele ya dharura au anapoitwa na kiongozi

(vii) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, picha za Viongozi wa Serikali , nembo ya Taifa na fedha za Taifa.

(viii) Mwanafunzi atatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.

(ix) Mwanafunzi anatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama anapoulizwa au kujibu swali darasani.

(x) Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani na asitoke nje bila ya ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.

(xi) Mwanafunzi kuwa au kumiliki simu ya mkononi endapo atakamatwa nayo itaharibiwa.

(xii) Mwanafunzi hataruhusiwa kumiki kifaa chochote kinachotumia umeme.

### 3.2 MAHUDHURIO

(i) Mwanafunzi atatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

(ii) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shughuli zote za elimu ya kujitegemea kama vile Kilimo, ufugaji na bustani.

(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba n.k.

### 3.3 MAANDALIO YA JIONI

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya jioni kuanzia saa 2.00 mpaka saa 4:00 usiku.

ii. Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote wa maandalio ya jioni hatakiwi kuwa na redio wala majadiliano ya vikundi

### 3.4 KUWAHI

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuthamini muda kwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule ya kila siku.

### 3.5 SARE YA SHULE

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni:-
   a) Suruali rangi ya dark bluu.

b) Shati nyeupe yenye nembo ya shule na yenye mikono mifupi
c) Viatu vyeusi vya ngozi na soksi nyeusi

(ii) Sare hii itavaliwa na mwanafunzi wakati wote wa:-
(a) Masomo ya darasani
(b) Kutoka nje ya shule kwa shughuli za shule
(c) Mhadara wa shule ( Baraza la shule)
(d) Anapokwenda Hospitalini
(e) Wanaposafiri kuja na kwenda nyumbani

(iii) Sare na mavazi yanayovaliwa na mwanafunzi shuleni yanatakiwa kuwa safi wakati wote.

## 3.6 MIPAKA YA SHULE

(i) Mwanafunzi ataonyeshwa mipaka ya shule
(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum
(iii) Mwanafunzi itabidi apate kibali maalum kama itabidi alale nje ya shule
(iv) Mwanafunzi haruhusiwi kutembea sehemu zifuatazo bila sababu maalum:-
(a) Chumba cha walimu ( Staffroom)
(b) Ofisi za shule
(c) Maabara
(d) Jikoni
(e) Nyumba za walimu na wafanyakazia wasio walimu
(v) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu zifuatazo:-
(a) Vilabu vya pombe
(b) Majumba ya starehe
(c) Majumba ya kufikia wageni

(vi) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya shughuli yoyote katika nyumba ya Ibada
(mfano kula, kulala, kusoma n.k) isipokuwa kuabudu tu kwa wakati maalum.

## 3.7 USAFI

Mwanafunzi azingatie usafi wake binafsi na mazingira ya shule kama vile mahali pa kulala (Bwenini) , vyoo, madarasa na maeneo yote yanayozunguka shule.

## 3.8 UKUMBI WA CHAKULA

(i) Mwanafunzi anatakiwa kula chakula katika ukumbi wa chakula na si sehemu nyingine yoyte, Wakati wa kula anapaswa kuwa ameketi chini.
(ii) Mwanafunzi atalazimika kufanya usafi siku ya zamu yake katika ukumbi wa chakula, maeneo ya ukumbi na vyombo vya kupakulia chakula.
(iii) Mwanafunzi haruhusiwi kula chakula jikoni.
(iv) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za heshima anapoingia ukumbi wa chakula, ni marufuku kuingia na taulo, mswaki, bukta n.k.

### 3.9 BWENINI

(i) Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake.
(ii) Mwanafunzi lazima awepo kwenye ukaguzi wa jumamosi
(iii) Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote katika mabweni wakati wote
(iv) Magari hayaruhusiwi kuingia katika sehemu ya mabweni
(v) Mwanafunzi atatakiwa kutunza mali aliyokabidhiwa bwenini na kuirejesha kila mwisho wa muhula.
(vi) Ni marufuku kupeleka viti, meza na chakula bwenini.

### 3.10 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(ii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iii) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(iv) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule
(v) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vi) Kufuga ndevu
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya,
(viii) Uvutaji sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xi) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
**(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.**
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

### 4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU:-

**a)** Fomu yz uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa ***Hospitali ya Serikali***. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakaporipoti Shuleni.
**b)** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
**c)** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.
**d)** Wasilisha kivuli cha cheti cha kuzaliwa
**e)** Wasilisha nakala ya karatasi ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne(**Result Slip**)

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

*KARIBU SANA KATIKA SHULE HII*

For: THE HEADMASTER
PUGU SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 9090
DAR ES SALAAM

**MKUU WA SHULE**

**Fomu maalum ya ukaguzi wa ukamilifu wa mahitaji muhimu**

Jina la Mwanafunzi ..................................darasa ........tarehe ya ukaguzi..................

1. **Risiti ya ada na michango mbalimbali**

2. Mahitaji muhimu mengineyo:

(i) Ream ya karatasi 1 ..........................
(ii) Vitabu vya masomo vya tahasusi husika........................
(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa biolojia..................
(iv) Scientific calculator..................
(v) Godoro la sponji **moja** futi **mbili na nusu** lenye foronya...............
(vi) Mashuka pair 2 rangi ya bluu bahari ( Light blue) futi 3/6, mto na foronya mbili ( rangi ya shuka) na chandarua 1...................
(vii) Vyombo vya Chakula (Bakuli, Sahani, Kijiko na Kikombe)................
(viii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko ..........................
(ix) Vifaa vya Usafi...................
(x) Taulo moja (1) mswaki, sabuni, na kanda mbili za kuogea pair 1.................
(xi) Sanduku la bati (1)....................
(xii) Picha nne(04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu. Mwanafunzi husika awe na passpot size (04) nne..............

3. Cheti cha kuzaliwa ....................
4. Medical Ecamination Form................
5. fomu ya maelezo binafsi....................
6. fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria................

Jina la mkaguzi ........................................................................

Sahihi ya mkaguzi ...................................

***Muhimu:** mwanafunzi hatapokelewa shuleni iwapo fomu hii haitakamilika.*

FOMU NA 1

**NAFASI YA KUENDELEA NA MASOMO YA SEKONDARI**

Mwanafunzi .............................................kidato cha .......mwaka .................

Nimefurahi kupokea nafasi iliyotajwa hapo juu aliyopewa mwanangu na nimeafiki kuwa aipokee. Nitajitahidi kumtimizia mahitaji ya muhinu kulingana na miongozo ya shule. Wakati wote nitakuwa tayari kusaidiana na uongozi wa shule katika kumlea kijana wangu.

Mimi.........................................................(Jina kamili mzazi/mlezi)

Umri............Kijiji ...........................Wilaya ya ...............................

Dini ....................................Uraia.......................Kazi ..............................
Anuani S.L.P.......................
...........................

Namba ya simu:.........................................,.......................................,...................

SAINI.................................

**3. MWENYEKITI / KATIBU WA KIJIJI**

Nathibitisha kuwa yote yaliyoandikwa na Mwanafunzi (jina)

............................................................................... na

Mzazi/ Mlezi (jina) .......................................Sahihi.......................

Jina la M/kiti Mtendaji wa kata..............................................

sahihi.......................................

Namba ya simu:.......................,.................................

Mhuri ...............................

**FORM NO. II**

## ILALA MUNICIPAL COUNCIL
## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(TO BE COMPETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER AND RETURNED TO THE HEADMASTER OF PUGU SECONDARY SCHOOL)

FROM..........................................................................
..........................................................................

Re: ......................................................................Age...............

Please examine the above named student and comment on his health by responding to the following items. Kindly put a tick in form of either YES or NO.

A. Does the student have problems in connection with

SIGHT .................. (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

HEARING (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

SPEECH ............... (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

T.B ............... (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

BLOOD PRESSURE (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

ANY PHYSICAL DISABILITY (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

STOOL ...................... (i) YES
(ii) NO

If YES state ..........................................................................

ANY OTHER FINDINGS ..........................................................................

B. DOCTOR'S RECOMMENDATION ..........................................................................

| ................................ | ................................ | ................................ |
|---|---|---|
| ***Name and signature*** | ***Designation*** | ***Station*** |

*FORM III*

*a) MAELEZO BINAFSI (HISTORIA FUPI YA MWANAFUNZI)*

**IZINGATIE**

1. **Historia fupi kuanzia kuzaliwa mpaka kusoma kwake**
2. **uwepo wa wazazi/ walezi**
3. **mazingira na makazi anayoishi.**
4. **mengineyo**

..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................

**b) Mkataba kati ya mwanafunzi na Shule**

Mimi ..................................................... wa kidato cha .............. mwaka............
Nikiwa na akili zangu timamu na bila kushawishiwa na mtu yeyote ninaahidi kwamba sitashiriki katika mgomo, fujo, jinai, na makosa mengine yoyote ya utovu wa nidhamu katika muda wote wa masomo yangu.
Mkataba huu umesainiwa leo tarehe......................mbele ya ........................................
Mkuu wa Shule, Pugu Sekondari.

........................................ ........................................................

**Saini ya mwanafunzi** **Saini ya Mkuu wa Shule**